East African Scholars Journal of Education, Humanities and Literature
OPEN ACCESS
*Abbreviated Key Title: East African Scholars J Edu Humanit Lit*
ISSN: 2617-443X (Print) & ISSN: 2617-7250 (Online)
Published By East African Scholars Publisher, Kenya
Volume-9 | Issue-4 | Apr- 2026 | DOI: https://doi.org/10.36349/easjehl.2026.v09i04.009

**Original Research Article**

# Mofu za Nafsi katika Muundo wa Kitenzi cha Lahaja ya Kimakunduchi

Amina Ali Khamis[1]*, Prof. Devet Goodness Sinyangwe[2], Dkt. Micheal Amiri Mashauri[3]
[1](Mwanafunzi wa shahada ya Uzamivu) Idara ya Lugha ya Kiswahili na Isimu, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam
[2](Mhadhiri Mwandamizi) Idara ya Lugha na Fasihi, Chuo Kishiriki cha Elimu cha Dar es Salaam
[3](Mhadhiri) Idara ya Lugha ya Kiswahili na Isimu, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam

**Article History**
**Received:** 27.02.2026
**Accepted:** 20.04.2026
**Published**: 27.04.2026

**Journal homepage:** https://www.easpublisher.com

**Quick Response Code**

**Abstract:** Mofu za nafsi ni vipashio vya msingi katika muundo wa vitenzi vya lugha za Kibantu. Dhima kuu ya mofu hizi ni kutoa upatanisho wa kisarufi kwa nomino au kiwakilishi mtenda au mtendwa katika tungo. Makala hii ilichunguza maumbo ya mofu za nafsi katika kitenzi cha lahaja ya Kimakunduchi. Uchunguzi huo umezingatia sifa za mofu hizo kimofofonolojia na kimofosintaksia. Katika viwango hivi mofu za nafsi zilichunguzwa katika mitindo na maumbo mbalimbali yaliyoathirika kifonolojia, ilhali hubeba dhima moja ya kimuundo na kiutendaji katika tungo husika. Pia mofu zilichunguzwa katika midhihiriko yake kimuonekano, kinafasi na kiutendakazi. Data za utafiti huu zilikisanywa kutoka shehia ya Nganani, Kibanguni na Kae-kuu kwa kutumia usimulizi na ushuhudiaji-shiriki. Utafiti huu ulitumia Nadharia ya Kanuni Finyizi iliyoasisiwa na Noam Chomsky (1995: 2000: 2001). Misingi mikuu ya nadharia hii ni umbo fonetiki na umbo mantiki ikimaanisha sauti na maana rejelewa ya sauti hizo zinazotokana na umilisi na utendaji wa wazawa. Katika kazi hii, mofu za nafsi hurejelewa kama vipatanishi vya kiima (Upk) au vipatanishi vya yambwa (Upy). Matokeo ya utafiti huu yanaonesha kuwa mofu za nafsi kama vipatanishi kiima na yambwa hudhihirika katika nafasi ya kiambishi awali katika kitenzi vikiwa katika hali ya dhahiri, mficho au jumuishi, kulingana na mazingira ya kifonolojia, kimuundo na umilisi wa wazungumzaji wazawa. Nafasi ya udhihirikaji wa mofu za nafsi ina athari muhimu za kimofosintaksia na kisemantiki.

**Keywords:** Nadharia Ya Kanuni Finyizi, Mofu Za Nafsi, Vipatanishi Kiima, Vipatanishi Yambwa, Mofu Fiche, Mofu Jumuishi.

**Copyright © 2026 The Author(s):** This is an open-access article distributed under the terms of the Creative Commons Attribution **4.0 International License (CC BY-NC 4.0)** which permits unrestricted use, distribution, and reproduction in any medium for non-commercial use provided the original author and source are credited.

## 1.0 UTANGULIZI

Lugha za Kibantu zimejengwa katika mifumo na sheria maalumu ya kimofolojia na kisintaksia. Mifumo ambayo kitenzi kinapewa nafasi ya kipekee kama mhimili wa uwasilishaji wa taarifa za kisarufi katika muundo wake. Moja ya vipengele muhimu vinavyounda muundo wa kitenzi katika lugha hizi ni mofu za nafsi, ambazo hubeba taarifa kuhusu mhusika mtenda, mtendwa au mtendewa wa kitendo katika tungo. Mofu hizi huchangia kwa kiasi kikubwa katika ufanisi wa upatanisho wa kisarufi katika ya vijenzi vya sentensi, hususan katika kitenzi, kiima na yambwa au yambiwa.

Watafiti wengi waliochunguza mofu za nafsi katika lugha nyingi za Kibantu, ikiwemo Kiswahili na lahaja zake, wamebaini kwamba licha ya kuwa kuna mfanano wa kisarufi katika lugha hizo, bado kuna tofauti ndogondogo za kisarufi na kimuundo katika udhihirikaji wa mofu za nafsi kati lugha na lugha. Mofu za nafsi zinaweza kuonesha mfanano au utofauti katika maumbo au nafasi baina ya lugha na lugha au lahaja na lahaja (taz, Vitale1981; Charwi 2019; Mwaipaja 2022;). Maumbo ya mofu na mabadiliko ya maumbo hayo kimatamshi hayaathiri utendakazi katika uundaji wa maana, mpangilio wa vijenzi vya tungo na uhalalishaji wa upatanisho wa kisarufi katika tungo husika.

Lahaja ya Kimakunduchi ni mojawapo ya lahaja za Kiswahili kinachozungumzwa kusini mwa kisiwa cha Unguja. Lahaja hii ni ambishi- bainishi kutokana na mofu zake zinaonesha sifa bainifu za kifonolojia, kimofolojia na kisintaksia kama ilivyo kwa lugha za Kibantu. Licha ya kuwa ni lahaja ya Kiswahili lakini inajisimamia katika upekee katika usarufi wa lugha. Utofauti huu hujitokeza wazi katika maumbo ya mofu yaliyomo n muundo wa kitenzi, hususan katika utamkaji wa sauti mbalimbali za mofu nafsi na udhihirikaji wa mofu za nafsi za kiima na yambwa katika vitenzi husika. Hali hii inaibua haja ya kufanya

uchunguzi mahsusi ili kubainisha maumbo ya mofu hizi, nafasi zake katika kitenzi na athari zake za kimofosintaksia.

Makala hii inalenga kuchunguza mofosintaksia ya mofu za nafsi katika kitenzi cha Kimakunduchi kwa kuzingatia upatanishi wa kisarufi wa kiima na yambwa. Uchunguzi huu unaongozwa na Nadharia ya Kanuni Finyizi chini ya Sarufi Zalishi, ambayo inasisitiza uchanganuzi wa maumbo ya mofu za nafsi na muundo wa mofu hizo kisarufi kwa kuzingatia kanuni za kimsingi na mazingira ya udhihirikaji wa mofu za nafsi katika lahaja ya Kimakunduchi. Kupitia nadharia hii, makala inaeleza namna mofu za nafsi zinavyodhihirika katika hali ya dhahiri, fiche au jumuishi, pamoja na sababu za kimuundo na kifonolojia zinazoathiri udhihirikaji huo.

Kwa jumla, makala hii inatarajiwa kuchangia katika taaluma ya isimu ya Kibantu kwa kuongeza maarifa kuhusu lahaja za Kiswahili, hususan Kimakunduchi, na kutoa mwanga mpya juu ya nafasi na dhima ya mofu za nafsi katika muundo wa kitenzi.

## 2.0 MAPITIO YA MAANDIKO

Tafiti mbalimbali zimeonesha kuwa mofu za nafsi ni vipengele muhimu katika muundo wa kitenzi cha lugha za Kibantu. Waandishi kama vile Barno (2013), Ngenzi (2016), Charwi (2019) na Mwaipaja (2022) wamebainisha kuwa vitenzi vya lugha za Kibantu hujengwa kwa vipashio kadhaa vinavyobeba taarifa za kisarufi kama nafsi, wakati, hali na ukanushi. Tafiti hizo, zimebainisha mofu za nafsi ya kwanza ya pili na ya tatu katika hali ya umoja na wingi. Licha ya mfanano wa mgawanyo wa mofu bado walitofautiana katika mgawanyo wa idadi ya maumbo ya mofu za nafsi na nafasi ya mofu za nafsi katika vitenzi vya lugha hizo (Kinandi; Kihehe; Kikuria; Kifipa). Tafiti zao hazihusiani moja kwa moja na makala hii lakini zimesaidia kwa kiasi kikubwa kwa kuwa ziligusia maumbo ya mofu (viwakilishi) za nafsi na kubainisha mofu hizo katika vitenzi vya lugha tajwa hapo juu.

Kwa upande wa vitenzi vya lugha ya Kiswahili, tafiti kama za Mohammed (2001), Vitale (1981), Kapinga (1983), Kihore na wenzake (2012) na Wasan-Chomi (2017), wamezichunguza mofu za nafsi kwa kina katika muundo wa kitenzi. Katika uchunguzi wao waligusia mofu nafsi kinafasi na kidhima kuwa kama vipatanishi vya kiima na vipatanishi yambwa. Matokeo ya tafiti zao yalionesha kuwa, mofu za nafsi hutokea katika nafasi maalumu kwenye kitenzi vya lugha ya Kiswahili. Udhihirikaji wa mofu hizo hauathiriwi na mazingira ya kisintaksia na kifonolojia. Hata hivyo, tafiti hizi zimejikita zaidi katika Kiswahili Sanifu kama lahaja ya Kiswahili iliyosanifishwa, hivyo kuacha pengo la kitaaluma katika lahaja nyingine kama Kimakunduchi.

Kuhusu lahaja Kimakunduchi, tafiti chache zilizopo, kama vile Iddi (2018), Hamadi (2018), Juma (2019) zimeangazia tofauti za kiisimu na za kimofolojia katika lahaja za Kiswahili kwa jumla. Walizigusia mofu za nafsi katika lahaja ya Kimakunduchi wakati walipoonesha mfanano na utofauti na lahaja nyingine kama vile Kipemba na Kitumbatu. Kulingana na upeo wa mada zao ilikuwa vigumu kuangazia kwa undani mofofonolojia na mofosintaksia ya mofu za nafsi katika kitenzi jambo lililofanywa katika Makala hii.

Kwa ujumla, mapitio haya yanaonesha kuwa, licha ya kuwepo kwa mchango mkubwa wa tafiti zilizotangulia kuhusu mofu za nafsi katika lugha za Kibantu, bado kuna pengo la maarifa kuhusu udhihirikaji wa mofu hizi katika lahaja za Kiswahili, hususan Kimakunduchi, ambalo ndilo pengo la kitaaluma linaloshughulikiwa katika makala hii.

### 1.0 Nadharia Iliyotumika

Makala hii imeongozwa na Nadharia ya Kanuni Finyizi iliyoasisiwa na Chomsky (1995, 2000, 2001) chini ya Sarufi Zalishi. Nadharia hii inalenga kueleza muundo wa lugha kwa kutumia kanuni chache za msingi zinazotokana na umilisi na utendaji wa wazungumzaji asilia, badala ya sheria nyingi za kimaelezo. Msingi mkuu wa nadharia hii ni dhana kwamba miundo ya kisarufi hujengwa kwa ufanisi wa hali ya juu ili kukidhi mahitaji ya umbo fonetiki (sauti za lugha) na umbo maantiki (maana rejelewa ya sauti hizo).

Katika muktadha wa nadharia hii, mofu za nafsi hutazamwa kama vipengele vyenye sifa za kisarufi vinavyohitaji kuthibitishwa na kuangaliwa katika maumbo na muundo katika vitenzi. Vipengele hivi hujitokeza katika nafasi za vichwa vya kirai, hususan kirai upatanishi kiima (KUpk) na kirai upatanishi yambwa (KUpy), ambavyo vina jukumu la kusimamia upatanisho wa kisarufi katika mofu za nafsi na uhusiano wa kimofosintaksia katika vijenzi vya tungo.

Chomsky pia anabainisha kuwa sifa za kifonolojia za vipashio vya kisarufi hutekelezwa katika kiwango cha umbo fonetiki, baada ya mahitaji ya kisintaksia kutimizwa. Hii ina maana kuwa, vipengele vya kisarufi vya mofu za nafsi vithibitishwe kimuundo, nadharia inaruhusu tofauti za kimaumbo au kifonolojia kujitokeza katika matamshi asilia. Dhana hii ndiyo msingi unaoruhusu kueleza udhihirikaji wa mofu za nafsi katika hali dhahiri, fiche au jumuishi bila kuvunja kanuni za usarufi.

Hoja za Chomsky zimeendelezwa na kushadidiwa na wataalamu wengine wa sarufi zalishi kama vile Baker (2008) na Radford (1997) wanaoonesha kuwa mabadiliko ya kimaumbo ya vipatanishi vya nafsi hayapaswi kutazamwa kama hitilafu za kisarufi, bali kama matokeo ya mwingiliano kati ya fonolojia, mofolojia na sintaksia katika kiwango cha umbo fonetiki. Pia wanasisitiza kuwa vipashio vya mofolojia, ikiwemo mofu za nafsi, vinaweza kubadilika kimaumbo kutokana na kanuni za athari za kifonolojia baada ya muundo wa kisintaksia kukamilika.

Katika utafiti huu, misingi mahsusi ya Nadharia ya Kanuni Finyizi iliyotumika ni pamoja na umbo fonetiki linaloangazia fonolojia, mofolojia na sintaksia ya maumbo ya mofu za nafsi kwa pamoja, na umbo matiki linaloangazia maana zinazoibuliwa za mofu hizo kulingana na wazawa wa lugha wenyewe. Kupitia misingi hii, makala imefanikiwa kuchunguza na kueleza mofosintaksia ya mofu za nafsi katika kitenzi cha lahaja ya Kimakunduchi kwa namna inayokidhi malengo ya utafiti na kutoa mchango katika taaluma ya isimu ya Kibantu. Baada ya ufafanuzi huu hatua inayofuata ni uchanganuzi wa data za utafiti huu.

## 4.0 Mofu Nafsi katika Kitenzi cha Kimakunduchi

Matokeo ya utafiti yanaonesha kuwa lahaja ya Kimakunduchi kama zilivyo lugha nyingi za Kibantu, mofu nafsi huwakilishwa na maumbo ya aina mbili, ambayo ni mofu huru na mofu funge. Mofu huru ambazo hujitokeza kama umbo huru kama hizi zifuatazo; *miye* "mimi" *suwe* 'sisi' *weye* 'wewe' *nyuwe* 'nyinyi' *yeye* 'yeye' *wawo* 'wao'. Mofu funge huambwikwa ndani ya kitenzi, kazi yake kuu ni kurejelea kima au yambwa ndani ya tungo. Mofu hizo zimejadiliwa na kuchanganuliwa kwa kutumia Kanuni ya Nadharia Finyizi.

Kwa mujibu wa Kanuni ya Nadharia Finyizi, mofu nafsi katika kitenzi huchanganuliwa kama upatanishi kiima (Upk) au upatanishi yambwa (Upy), inayowakilishwa kwa kiwakilishi nafsi au ngeli kutegemea kundi la nomino inayopatanishwa nayo ilivyotumika katika tungo husika. Pia, ubainishaji wa mofu hizo hujumuisha uchanganuzi wa mazingira ya utokeaji wake. Wakati mwingine mofu hizo husababisha mabadiliko baina ya umbo la mofu na sauti zilizojengeka kwa wamilisi, kwenda katika midhihiriko wazi kiutendaji kwa kutamkwa na inavyotafsiriwa na wasikilizaji. Midhihiriko hiyo inatokana na umbo fonetiki (kiwakilishi fonolojia, mofolojia na sintaksia) na umbo mantiki (kiwakilishi cha maana rejelewa) kwa wamilisi wa lugha husika kikiwamo Kimakunduchi. Maumbo ya mofu za nafsi hizo yamejadiliwa na kuchanganuliwa katika vipengele 3.1, 3.2 na 3.3.

Zaidi ya hayo, uchanganuzi umezingatia mazingira ya fonolojia, mofolojia na sintaksia yanayoathiri namna mofu hizo zinavyodhihirika katika usemi. Wakati mwingine, kutokea kwa mofu hizo huzua mabadiliko ya kifonetiki na kimaumbo, ambayo haiathiri midhihiriko ya kidhana na kimaana kwa watumiaji wa lahaja ya Kimakunduchi. Kwa hivyo, mofu za nafsi huchambuliwa si tu kama vipashio vya kifonolojia, bali pia kama vielelezo vya maana rejelewa vinavyofungamana na muktadha wa matumizi ya lugha, mabadiliko hayo yametolewa ufafanuzi kupitia majedwali Na.1 na 2. Baada ya kuangalia mofu nafsi kwa ujumla, kipengele cha 3.1 kimeangalia mofu nafsi ya kwanza.

## 4.1 Mofu za Nafsi ya Kwanza

Matokeo ya utafiti yanaonesha kuwa katika lahaja ya Kimakunduchi mofu za nafsi, ambazo huambatishwa moja kwa moja kwenye vitenzi; nafsi ya kwanza umoja huwakilishwa na mofu {*ni*-} na {*nyi*-}, wakati nafsi ya kwanza ya wingi huwakilishwa na mofu {*wa*-}. Mofu {*ni*-} hujumuishwa kama fonimujumuishi [*N*], ambayo hubadilika kulingana na mazingira ya kifonolojia, hususani sauti ya awali ya shina la kitenzi. Mabadiliko haya husababisha kuibuka kwa maumbo mbalimbali ya {*ni*-}, yanayojulikana kitaalamu kama alomofu.

Vilevile, mofu {nyi-} pia hujitokeza kwa njia tofauti kama {*nyi*-} au {*ny*-}, mabadiliko haya yakisababishwa na udondoshaji wa irabu /i/ pale ambapo shina la kitenzi huanza na irabu kama /a/, /e/, /i/, au /o/. Mabadiliko haya ni matokeo ya mchakato wa kifonolojia unaosawazisha ugeuzi wa matamshi katika usemi wa kawaida.

Maumbo haya ya alomofu, ambayo huakisi mwingiliano wa mofu na mazingira yake ya kifonolojia, yamewasilishwa kwa muhtasari katika Jedwali Na.1, ili kuonesha utofauti wa kimaumbo unaosababishwa na mazingira ya kisarufi na kifonolojia. Tuchunguze maumbo hayo ambayo yanayojulikana kama alomofu katika Jedwali Na. 1.

**Jedwali Na.1: Midhihiriko ya Alomofu Mbalimbali za $Nfs_{1u}$ katika Kimakunduchi**

| Na. | Mofu $Nfs_{1u}$ | Mifano katika Vitenzi | Tafsiri ya Kiswahili Sanifu |
|---|---|---|---|
| 1. | *n'g*- [ŋ] | ***ng'*** *– kutu* | 'nimekuta/ nilikuta' |
| 2. | *m*- [ɱ] | ***m*** *–fagii* | 'nimefagia/ nilifagia' |
| 3. | *n*- | ***n-*** *somo* | 'nimesona /nilisoma' |
| 4. | *nya*- | ***ny*** *– angasa* | 'nimefukuza/ nilifukuza' |
| 5. | *nye*- | ***ny*** *– ende* | 'nimekwenda/nilikwenda' |
| 6. | *nyo*- | ***ny*** *– oso* | 'nimekosha/nilikosha' |
| 7. | *nyi*- | ***nyi-****uku* | 'nimeondoka/niliondaka' |
| 8. | *Ø* | *-cha – cheza* | 'nitacheza' |
| 9. | *Ø* | *-ha- lya* | 'nikala' |
| 10. | *Ø* | *-na - vika* | 'ninapika' |

**Chanzo**: Data za Uwandani (2022)

Kama inavyooneshwa katika Jedwali Na.1, mofu za nafsi ya kwanza umoja (Nfs1u) katika Kimakunduchi hujidhihirisha kwa maumbo mbalimbali kama *nyi-*, *nya-*, *nye-*, *nyo-*, *n-*, *n'g*, *m'*, na *Ø*. Mabadiliko haya ya maumbo yanasababishwa na michakato ya kifonolojia kama vile udondoshaji na usilimishaji. Mofu {nyi-}, ambayo huwakilisha nafsi ya kwanza umoja, hupitia mchakato wa udondoshaji wa irabu /i/ pale ambapo shina la kitenzi likianza na irabu, hivyo kutoa maumbo kama *nya-*, *nye-*, *nyo-* au *nyi-* kulingana na irabu husika.

Aidha, umbo kapa {Ø} hujitokeza pale ambapo mofu {ni-} ya nafsi ya kwanza hudondoshwa kwa sababu ya kuwepo kwa mofu za njeo kama *{cha-}* (ya wakati ujao), *{na-}* (ya wakati uliopo), au *{ha-}* (ya wakati uliopita kimasimulizi), ambapo mofu ya nafsi hubakia kimya kimatamshi lakini huendelea kutenda kazi yake kisarufi. Kwa mujibu wa Ndharia ya Kanuni Finyizi kupitia kanuni ya uwekevu wamilisi wa lugha huweza kuficha au kuwacha baadhi sauti kwa lengo la uchumi wa lugha na urahisishaji wa matamshi, hasa katika matumizi ya wazungumzaji wazawa.

Vilevile, mofu ya nafsi ya kwanza huwa na umbo jumuishi {*N-*}, ambalo husilimishwa kulingana na konsonanti (silabi) ya kwanza ya shina la kitenzi, hali inayozalisha alomofu zenye sauti kama [*m-*, *n-*, *ŋ-* (n'g) na *ɱ-]*. Ufafanuzi wa kina wa michakato hii umetolewa katika maelezo yanayofuata, yakiegemea mifano ya uteuzi wa wazungumzaji asilia kama ilivyotolewa katika Jedwali Na. 2.

**Jedwali Na. 2: Michakato ya Udondoshaji wa Irabu /i/ na Mofu Nfs$_{1u}$ {ni-}**

| **Na.** | **Mofu Nfs$_{1u}$** | **Umilisi wa wazawa** | **Michakato ya kifonolojia** | **Utendaji wa wazawa** | **Maana rejelewa** |
|---|---|---|---|---|---|
| **1.** | *ny-* | *nyi-angas-a* | *udondoshaji wa sauti ya irabu /i/* | *nyangasa* | nimefukuza |
| **2.** | *ny-* | *nyi- end-e* | *udondoshaji wa sauti ya irabu /i/* | *nyende* | nimekwenda |
| **3.** | *nyi-* | *nyi- os-o* | *udondoshaji wa sauti ya irabu /i/* | *nyoso* | nimekosha |
| **4.** | *ni-* | *ni- na-vik-a* | *udondoshaji wa sauti ya mofu nafsi {ni}* | *ønavika* | ninapika |
| **5.** | *ni-* | *ni- cha-kwim-a* | *udondoshaji wa saiuti ya mofu nafsi{/ni}* | *øchakwima* | nitasimama |
| **6.** | *ni-* | *ni- ha- chez-a* | *udondoshaji wa sauti ya mofu nafsi {ni}* | *øhavika* | nikapika |

**Chanzo:** Data za Uwandani (2022)

Uchunguzi wa mifano iliyowasilishwa katika Jedwali Na.2 unaonesha wazi mchakato wa udondoshaji unaoathiri mofu {*nyi-*} na {*ni-*} katika lahaja ya Kimakunduchi. Mofu {*nyi-*} hupitia udondoshaji wa sauti ya irabu /i/, hususani pale ambapo shina la kitenzi linaanza na irabu katika mfano (1-3). Hali hii huibua alomofu kama *ny-*, ambazo huchukua irabu ya kwanza ya kitenzi husika, mathalan katika vitenzi *nyende* 'nimekwenda', *nyoso* 'nimeosha', na *nyangasa* 'nimefukuza'.

Kadhalika, sauti ya mofu {*ni-*} hupitia mchakato sawa wa udondoshaji katika mazingira ya njeo mbalimbali, kama vile *cha-* (wakati ujao), *na-* (wakati uliopo), na *ha-* (wakati uliopita kimasimulizi), kama inavyojitokeza katika vitenzi kama *chakwima* 'nitasimama', *navika* 'ninapika' na *havika* 'nikapika'. Ingawa sauti ya mofu ya nafsi haitamkwi moja kwa moja, inabakia kutekeleza majukumu yake ya kisarufi, hivyo kudhihirisha uamilifu wake katika mfumo wa sentensi. Hili linaonesha uwezo wa kifonolojia kubadilisha sauti ya umbo la mofu bila kuathiri kazi yake katika tungo.

Vilevile, maumbo *n, m na n'g* yamesababishwa na mchakato wa usilimisho wa fonimujumuishi /N-/, ambayo hujidhihirisha kwa sura mbalimbali za nazali. Kulingana Chomsy 2000, alisisitiza uchanganuzi wa maumbo ujikite zaidi kwa wamilisi wa lugha asilia ili kuelewa wanasema vipi na wanamaanisha nini. Nadharia imesisitiza tunapoangalia umbo fonetiki na umbo mantiki tuangalie umilisi na utendaji wa wanalugha, tuangalie Data Na.1 kwa ufafanuzi zaidi.

(i) ***n*** - *fukiz- i* usilimisho/ni/→ *m- fukiz-i* 'nimefukiza / nilifuka'Nfs$_{1u}$ M$_{zz}$ Nj$_{Pt}$/H$_{lt}$

(ii) ***n*** *-vik-i* *usilimisho/ni/→* *m-vik-i* 'nimepika/ nilipika' Nfs$_{1u}$ M$_{zz}$ Nj$_{Pt}$/H$_{lt}$

(iii) ***ni****- tamb-u* → *usilimisho/ni*/ *n- tamb-u* 'nimejua/ nilijua' Nfs$_{1u}$ Mzz Hlt

(iv) ***ni****-zo-o* → *usilimisho/ni/* *n-zo-o* 'nimezoa/ nilizoa' Nfs$_{1u}$ Mzz Hlt

(v) ***ni****-som-o* /→ *usilimisho/ni*/ *n- som-o* 'nimesoma/ nilisoma'Nfs$_{1u}$ Mzz Hlt

(vi) ***ni****-kos-o* *usilimisho/ni*/→ *n'gkoso* 'nimekosa'Nfs$_{1u}$ Mzz Hlt

**Chanzo:** Data za Uwandani (2022)

Data Na.1 inadhihirisha kwa ufasaha michakato ya kifonolojia ya usilimishaji wa fonimujumuishi /*N*/ katika mazingira mbalimbali ya kifonetiki ya lahaja ya Kimakunduchi. Michakato hii husababisha kutokea kwa maumbo tofauti ya nazali, kulingana na tabia fonolojia ya fonimu inayofuata katika kitenzi husika. Hali hii inaakisi kanuni za kifonolojia za upatanisho wa kisarufi kwa mahali pa kutamkia, ambapo mofu ya nafsi ya kwanza umoja {ni-} hubadilika kulingana na mazingira ya sauti inayofuatana nayo.

Katika mifano (i) na (ii), usilimishaji wa /*N*/ umezaa sauti [ɱ] inayoakisiwa na alomofu *m-* katika vitenzi *mfukizi* 'nimefukiza' na *mviki* 'nimepika'. Hali hii inajitokeza pale ambapo fonimu ifuatayo ni ya

umidomo (mdomo-meno), kama /f/ na /v/, ambazo hutamkwa kwa mguso wa meno ya juu na mdomo wa chini, hivyo kuathiri namna nazali inavyotamkwa.

Mifano (iii) hadi (v) unaonesha kuwa sauti /ni-/ imesilimishwa kwa kutamkwa kama sauti ya nazali ya ufizi kuwa [n-] katika vitenzi *ntambuu* 'nimejuwa', *nsomo* 'nimesoma' na *nzoo* 'nimezoa'. Hii inamaanisha kuwa fonimujumuishi /*N*/ imetokea kama sauti [n] katika mazingira ya kufuatiwa na fonimu zenye sifa ya kutamkwa kwenye ufizi.

Katika mfano wa sita (vi), tunashuhudia fonimujumuishi /*N*/ imesilimishwa kuwa [ŋ] katika kitenzi *n'gkoso* 'nimekosa'. Hii inamaanisha kuwa fonimujumuishi /*N*/ imetokea kama [ŋ] katika mazingira ya kufuatiwa na fonimu zenye sifa ya kutamkwa kwenye kakaa laini.

Kwa hivyo, michakato hii ya kifonolojia siyo tu inabainisha kuwepo kwa mofu ya nafsi, bali pia inadhihirisha namna mofu hizo zinavyobadilika kimazingira huku zikibaki na utendakazi wake wa kisarufi, na hivyo kuonesha upekee wa Kimakunduchi katika mfumo wa uundaji wa vitenzi.

Kwa upande mwingine katika lahaja ya Kimakunduchi kuna nafsi ya kwanza wingi ($Nfs_{1w}$) ambayo huwakilishwa kwa mofu {*tu*} kama inavyojitokeza katika Data Na. 2

(i) *tu- cha- lyavy- a* 'tutatoa' $Nfs_{1w}$ $Nj_{jo}$ $M_{zz}T_{mt}$
(ii) *tu- lipiz- i* 'tumelipiza/ tulilipiza' $Nfs_{1w}$ $M_{zz}$ $Nj_{pt}/T_{mt}$
(iii) *tw- end-e* 'tumekwenda/ tulikwenda' $Nfs_{1w}$ $M_{zz}Nj_{pt}/T_{mt}$
(iv) *tw-ish-i* 'tumekwisha/ tulikwisha' $Nfs_{1w}$ $M_{zz}$ $Nj_{pt}/T_{mt}$
(v) *tw-akw-a* 'tumepewa'/ tulipewa $Nfs_{1w}$ $M_{zz}$ $Nj_{pt}/T_{mt}$

**Chanzo:** Data za Uwandani (2022)

Data Na. 2 hapo juu inaonesha mofu za nafsi ya pili inavyowakilishwa na umbo {*tu*} au {*tw*}. Katika mifano (i) na (ii), mofu ya Nfs1w hujitokeza kwa umbo lake la msingi {tu-} mbele ya vitenzi ambavyo mashina yake yanaanza na konsonanti. Hii inabainisha kuwa katika mazingira ambayo hakuna mzozano wa kifonolojia baina ya irabu ya mofu na sauti ya mwanzo ya shina, mofu hudhihirika kwa umbo lake kamili bila mabadiliko.

Hata hivyo, mifano (iii), (iv) na (v) inaonesha kuwa mofu hiyo hiyo ya msingi hubadilika na kuwa {tw-} inapowekwa kabla ya vitenzi vinavyoanza na irabu. Hii ni kutokana na mchakato wa uyeyushaji wa irabu /u/, ambapo irabu hiyo hubadilika na kuwa kiyeyushi cha mdomo /w/ inapokutana na irabu nyingine isiyofanana nayo, ili kuepusha muingiliano wa irabu mbili mfululizo. Hali hii inajitokeza katika vitenzi kama *twende* 'tumekwenda', *twishi* 'tumekwisha', na *twakwa* 'tumepewa', ambapo /w/ hufanya kazi ya kupatanisha mpishano wa kifonolojia kati ya mofu na shina la kitenzi.

Kwa hivyo, uteuzi wa maumbo {*tu-*} na {*tw-*} katika Kimakunduchi ni matokeo ya kanuni maalum za kifonolojia zinazolenga kuhakikisha ufasaha na urahisi wa matamshi. Mabadiliko haya yanasisitiza mwingiliano wa karibu kati ya sarufi na fonolojia katika uundaji wa maneno ya Kiswahili cha Kimakunduchi. Baada ya uchambuzi wa mofu nafsi ya kwanza, hatua inayofuata ni uchanganuzi wa mofu nafsi ya pili.

**4.2 Mofu za Nafsi ya Pili**

Katika Kimakunduchi, nafsi ya pili huwasilishwa kwa njia mbili kuu: mofu huru na mofu funge. Mofu huru kama *weye* kwa umoja 'wewe' na *nyuwe* kwa wingi 'nyinyi' hutumika zaidi katika mazungumzo ya moja kwa moja. Kwa upande mwingine, katika kitenzi, nafsi hii huwakilishwa na mofu funge {ku-} au {u-} kwa umoja, na {m-}, {mu-} au {mw-} kwa wingi. Uchambuzi wa data unaonesha kuwa mofu hizo hujitokeza katika miundo ya vitenzi kwa namna mbili: ya kwanza ikiwa kama kiima katika nafasi ya awali ya kitenzi, na ya pili ikiwa kama yambwa – yaani, katika nafasi ya karibu na mzizi wa kitenzi.

Uchunguzi wa matumizi ya mofu {ku-} unaonesha kuwa hutumika sana katika kusemezana na mtu wa pili, ambapo msemaji anaweza kuwa anatoa taarifa au anauliza swali. Muktadha wa mazungumzo pamoja na kiimbo cha matamshi hutumika kutofautisha kama kitenzi ni taarifa au swali. Katika hali ya kawaida ya mazungumzo ya kila siku, kitenzi kinaweza kuwa na dhima mbili kulingana na mazingira ya matumizi. Kwa mfano, sentensi kama *kunyono* inaweza kumaanisha 'umeniona' ikiwa kama taarifa, au 'umeniona?' ikiwa kama swali, kulingana na kiimbo au lafudhi ya msemaji. Data Na. 3 inadhihirisha muundo huu kwa ufasaha:

(i) *ku- ny- on- o* 'umeniona' $Nfs_{2u}$ $Nfs_{1u}$ $M_{zz}$ $Nj/T_{mt}$
(ii) *ku- sumk- u* 'umekimbia' $Nfs_{2u}$ $M_{zz}$ $T_{mt}$
(iii) *ku- lamk- u* 'umeamka' $Nfs_{2u}$ $M_{zz}$ $T_{mt}$
(iv) *ku- kos-o* 'umekosa' $Nfs_{2u}$ $M_{zz}$ $T_{mt}$

**Chanzo:** Data za Uwandani (2022)

Katika mifano ya Data Na. 3 hapo juu, mofu ya $Nfs_{2u}$ {ku-} inaonekana waziwazi kama kiima katika nafasi ya awali ya kitenzi. Mfano wa (i) ni wa kipekee kwa kuwa unaonesha pia matumizi ya mofu ya yambwa {-ny-}, inayodokeza nafsi ya kwanza umoja ($Nfs_{1u}$), ikionesha kwamba kitendo hicho kimemlenga msemaji. Mzizi wa kitenzi {-on-} humaliziwa na irabu tamati /o/, inayochukua kazi ya kuonesha hali timilifu ya tendo hilo.

Katika mifano mingine iliyobaki (iii-v) mofu ya $Nfs_{2u}$ {*ku-*} imefuatiwa na mzizi wa kitenzi kisha irabu tamati iliyobeba dhima ya hali timifu. Vitenzi hivyo vimeonesha kubadilisha nafasi ya njeo au hali kutoka nafasi ya mwanzo kabla ya mzizi (kama zilivyo lugha nyingi za Kibantu) kwenda nafasi ya mwisho, yaani baada ya mzizi. Irabu tamati za vitenzi hivyo hubadilika

kulingana na irabu iliyomo kwenye mzizi wa kitenzi. Hii ina maana kuwa kwenye lugha ya Kimakunduchi hakuna urari wa irabu tamati katika vitenzi inayowakilisha njeo ya wakati uliopita au hali timilifu kama zilivyokuwa lugha nyingi za Kibantu.

Aidha, mfano wa kitenzi katika (ii) mofu {*ku-*} imejitokeza nafasi ya mwanzo na kufuatiwa na mofu ya wakati uliopo {*-na-*}, mzizi wa kitenzi {*-tend-*}na kumalizia na irabu tamati /a/. Muundo huu unaonesha kuwa vitenzi vinadhihirisha njeo ya wakati katika nafasi ya kiambishi awali huwa ina mofu tamati /a/ kama zilivyo lugha nyingi za Kibantu. Hata hivyo, mofu hiyohiyo inapokutana na vitenzi vilivyoanza kwa irabu, basi irabu yake huathirika na kudhihirika katika umbo tofauti kama zilivyojitokeza kwenye nafsi nyingine zilizotangulia.

Vilevile, uchambuzi wa data umeonesha kuwa $Nfs_{2u}$ katika Kimakunduchi pia huwakilishwa kwa mofu {*u-*}. Tuchunguze Data Na. 4 kwa ufafanuzi zaidi.

(i) *u- k –end-* a 'ukienda' $Nfs_{2u}U_{Sh}M_{zz}T_{mt}$
(ii) *u- ka- vit-a* 'ukipita' $Nfs_{2u}U_{Sh}M_{zz}$ $T_{mt}$
(iii) *u- sem- e* 'useme' $Nfs_{2u}$ $M_{zz}$ $T_{mt}$
**Chanzo:** Data za Uwandani (2022)

Mfano wa Data Na. 4 unaonesha mofu ya $Nfs_{2u}$ {*u-*} mara nyingi hutumika katika taarifa zenye ushuruti wa jambo ambalo linahitaji kujalizwa ili taarifa itimie kwa anayepewa agizo hilo. Katika mfano wa (i) na (ii) mofu {*u-*} imefuatana na mofu ya ushuruti {*ka-*} na kufuatiwa na shina la kitenzi kinachohusika. Kadhalika, katika mifano ya (iii) mofu {*u-*} imefuatiwa na mzizi wa kitenzi na kumaliziwa na irabu tamati. Utafiti huu ubainisha mofu hizi za $Nfs_{2u,}$ alomofu zake zinazoweza kuwa zimegawana mazingira ya utokeaji wake kuwa {*u-*} hujitokeza kwa vitenzi vya amri na vyenye mofu za ushurutu {*ka-*} 'ki'. Pia kwa upande wa mofu {*ku-*} hujitokeza katika vitenzi venye njeo za wakati uliopo, ujao na uliopita.

Katika lahaja ya Kimakunduchi, nafsi ya pili wingi ($Nfs_{2w}$) huwasilishwa kwa mofu mbalimbali: {m-}, {mw-}, na {mu-}. Mofu hizi ni alomofu za mofu msingi {mu-}, na hutofautiana katika utokeaji kulingana na mazingira ya kifonolojia na kimaumbo ya vitenzi husika. Uchambuzi wa data zilizokusanywa kutoka uwandani unaonesha kuwa alomofu hizi hutokea kwa mtiririko wa kimuktadha, zikifuatilia kanuni za ulinganifu wa kifonolojia na urahisi wa matamshi. Data Na. 5 inatoa ushahidi wa namna alomofu hizi zinavyotokea:

(i) ***m*** *- sha- mu- uz - a?* 'mshamuuliza?' $Nfs_{2w}$ $H_l$ $Nfs_{3u}$ $M_{zz}$ $T_{mt}$
(ii) ***m****- pig- an- e* 'mpigane' $Nfs_{2w}$ $M_{zz}$ $K_{ulAN}$ $T_{mt}$
(iii) ***mu-*** *m- kut- u* 'mmemkuta' $Nfs_{2w}$ $Nf_{3u}$ $M_{zz}$ $H_{lT}$
(iv) ***mu****-ya-gom-o* 'mmeyaweza' $Nfs_{2w}$ $N_{g6}$ $M_{zz}H_{LT}$
(v) ***mw****- angas -e* 'mfukuze' $Nfs_{2w}$ $M_{zz}$ $T_{mt}$
(vi) ***mw****- ap-e* 'mtafuta' $Nfs_{2w}$ $M_{zz}$ $T_{mt}$
**Chanzo:** Data za Uwandani (2022)

Katika Data Na. 5, mifano ya (iii) na (iv), mofu ya msingi ya $Nfs_{2w}$ {mu-} imejitokeza kikamilifu, hasa katika mazingira ya wakati uliopita au hali timilifu, ambapo mofu ya yambwa huambatana nayo. Katika mazingira haya, utelezi wa matamshi huruhusu irabu /u/ ya mofu kuendelea kuwepo.

Hata hivyo, katika mifano ya (i) na (ii), ambapo vitenzi vipo katika njeo ya wakati uliopo, ujao au hali ya utendeaji (kama amri au hali tegemezi), irabu /u/ ya mofu {mu-} hudondoshwa kutokana na shindikizo la kifonolojia ili kupunguza mzigo wa matamshi. Hali hii huibua alomofu {m-}, ambayo ni matokeo ya mchakato wa udondoshaji kwa ajili ya ufasaha na urahisi wa kimatamshi wa sauti.

Aidha, mifano ya (v) na (vi) inaonesha matumizi ya alomofu {mw-}, ambapo mofu ya msingi {mu-} huambikwa kwenye vitenzi vinavyoanza na irabu. Katika mazingira haya, irabu ya mwisho ya {mu-} hubadilika kuwa konsonanti ya kiyeyusho cha midomo /w/, hivyo kuzalisha {mw-}. Mabadiliko haya yanafuata kanuni za kifonolojia ya uyeyushaji, ambapo kuingiliana kwa irabu mbili huepukwa kwa kutumia konsonanti ya mdomo ili kurahisisha mtiririko wa matamshi.

Kwa hivyo, uchunguzi huu unadhihirisha kuwa mofu {mu-} ni ya msingi katika uwakilishi wa $Nfs_{2w}$, huku {m-} na {mw-} zikiwa ni alomofu zinazochochewa na mazingira ya kifonolojia na muktadha wa sintaksia ya kitenzi. Ubadilikaji huu ni ushahidi wa ubunifu na ufanisi wa mifumo ya kifonolojia ya lahaja ya Kimakunduchi katika kudumisha uwiano wa kisarufi na urahisi wa mawasiliano. Baada ya uchanganuzi wa mofu nafsi ya pili kipengele kinachofuata ni uchanganuzi wa mofu nafsi ya tatu.

### 4.3 Mofu za Nafsi ya Tatu

Katika lahaja ya Kimakunduchi, nafsi ya tatu huwakilishwa kwa maumbo mbalimbali ya mofu funge yanayobeba dhima ya muundo wa kiima ndani ya kitenzi. Katika umoja, mofu hizo hujitokeza kama {ka-}, {a-}, {mwa-}, na {m-}, ilhali katika wingi huwakilishwa na {wa-}. Jedwali Na.3 linabainisha matumizi ya mofu hizo kulingana na muktadha wa kisintaksia na kimofolojia, na hutoa msingi wa uchambuzi wa maumbo ya nafsi ya tatu katika jahaja ya Kimakunduchi.

**Jedwali Na. 3: Maumbo Mbalimbali ya Mofu za Nafsi ya Tatu**

| Na. | mofu za nafsi | Mfano waVitenzi | Tafsiri ya Kiswahili |
|---|---|---|---|
| 1. | *ka-* | *ka-sem-e* <br> *$Nfs_{3u}$ $M_{zz}H_{LT}$* | 'amesema' |
| 2. | *a-* | *a-vo-kufw-a* <br> *$Nfs_{3u}$ $RejM_{zz}T_{mt}$* | 'alipokufa' |
| 3. | *m-* | *m-na- kukw-a* <br> *$Nfs_{3u}$ $Nj_{po}(Rej)M_{zz}T_{mt}$* | 'anayepewa' |
| 4. | *mwa-* | *mwa-sumk-a* <br> *$Nfs_{3u}$ $(N_{jpt}Rej)M_{zz}T_{mt}$* | 'aliyekimbia' |
| 5. | *wa-* | *wa-u-kut-u* <br> *$Nfs_{3w}Ng_{11}M_{zz}$ $T_{mt}$* | 'wameukuta' |

**Chanzo:** Data za Uwandani (2022)

Jedwali Na. 3 linaonesha mofu nafsi funge za nafsi ya tatu umoja na wingi kama zinavyobainika katika lahaja ya Kimakunduchi. Mifano minne ya mwanzo (1-4) inadokeza mofu za nafsi ya tatu umoja ($Nfs_{3u}$) na mfano wa (5) unadokeza mofu za nafsi ya tatu wingi ($Nfs_{3w}$).Tuangalie mofu hizo moja baada nyingine, tunaanza na {*ka-*} inavyodhihirika katika vitenzi kwenye Data Na. 6.

(i) (i) *ka- u- kut- u* 'ameukuta/ aliukuta' $Nfs_{3u}$ $N_{g11}M_{zz}$ $H_l$ /$T_{mt}$
(ii) *ka- chom- o* 'amechoma/ alichoma' $Nfs_{3u}$ $M_{zz}$ $H_l$/$T_{mt}$
(iii) *k- os- o* 'amekosha/alikosha' $Nfs_{3u}$ $M_{zz}$ $H_l$/$T_{mt}$
(iv) *k- enjk-I* 'ameinjika / aliinjika' $Nfs_{3u}$ $M_{zz}$ $T_{mt}$
(v) *k e-me- ji-uzul- u* 'amejiuzulu' $Nfs_{3u}$ $H_l$ $J_t$ $M_{zz}$ $T_{mt}$

**Chanzo:** Data za Uwandani (2022)

Katika Data Na. 6, mifano (i) na (ii), mofu ya $Nfs_{3u}$ imejitokeza kikamilifu kwa umbo lake la msingi {ka-}, hasa pale ambapo kitenzi kinachoambatanishwa nacho kinaanza na konsonanti (kama katika *ka-chomo*) au irabu kama /u/ au /a/ (kama katika *ka-ukutu*). Hii inaashiria kuwa hakuna mgongano wa kifonolojia unaolazimu mabadiliko ya umbo la mofu hiyo.

Hata hivyo, mabadiliko hujitokeza katika mazingira mengine. Katika mfano wa (iii) *k-os-o* 'amekosha' na (iv) *k-enjik-i* 'ameinjika', ambapo mzizi wa kitenzi unaanza na irabu kama /o/ na /e/, mchakato wa udondoshaji wa irabu /a/ kutoka kwenye mofu {ka-} hutokea. Hili ni tokeo la kanuni ya fonolojia inayojiepusha na mkusanyiko wa irabu mbili, hivyo kurahisisha matamshi kwa kudondosha irabu ya kwanza na kuruhusu irabu ya pili (ya mzizi) kuchukua nafasi ya awali. Kwa hiyo, mofu ya {ka-} hubadilika na kuwa {k-}, ambayo ni alomofu ya mofu hiyo ya msingi.

Katika mfano wa (v), ambapo tunapata umbo la {ke-} kama katika *ke-me-jiuzulu*, mabadiliko haya yanadhihirisha mvutano wa kifonolojia wa irabu, ambapo badala ya kudondoshwa kabisa, irabu ya mofu ya msingi hubadilishwa kuwa ile inayolingana zaidi na irabu ya mzizi, ili kurahisisha uunganishaji wa silabi. Mabadiliko haya ni sehemu ya mchakato wa utangamano wa irabu, unaolenga kudumisha mtiririko wa silabi unaopendelewa katika fonolojia ya lahaja ya Kimakunduchi.

Kwa hivyo, mofu ya nafsi ya tatu umoja {ka-} ni mofu yenye ubadilifu wa kifonolojia unaochochewa na mazingira ya sauti ya mzizi wa kitenzi. Alomofu zake {k-} na {ke-} ni vielelezo vya unyumbufu wa kifonolojia unaolenga urahisi wa matamshi na ufasaha wa lugha. Uchambuzi huu unaonesha namna Kimakunduchi kinavyodumisha kanuni za kifonolojia bila kupoteza maana ya kisarufi, na hivyo kudhihirisha ubunifu wa muundo wa vitenzi wa lugha hii.

Vilevile, nafsi ya tatu umoja ($Nfs_{3u}$) huwakilishwa na {ke} pale {*ka-*} inapofuatiwa na sauti /i/. Hii ina maana kuwa hutokea mchakato wa kifonolojia wa mvutano wa irabu uliosababishwa na irabu ya chini /a/ kuvutana na irabu ya juu /i/ na kupatikana irabu ya kati /e/ kama ilivyojitokeza katika kitenzi kwenye mfano wa (iv) na mifano ya vitenzi vyingine kama zilivyodhihirika katika Data Na. 7.

(i) *ka-im-i* mvutano wa irabu /a+ i /→ /e/→ *kemi* 'amesimama' $Nfs_{3u}$ $M_{zz}$ $T_{mt\ chini+juu}$→ kati
(ii) *ka- igiz-i* mvutano wa irabu / a+ i/ →/e/→ *kegizi* 'ameigiza' $Nfs_{3u}$ $M_{zz}$ $T_{mt\ chini+juu}$→ kati
*(iii) ka –imb-i* mvutano wa irabu / /a+ i/ →/e/→ *kembi* 'ameimba' $Nfs_{3u}$ $M_{zz}$ $T_{mt\ chini+juu}$→ kati

**Chanzo:** Data za Uwandani (2022)

Aidha, Data Na.7 hapo juu, mifano yake yote inaonesha nafsi ya tatu umoja ($Nfs_{3u}$) imedokezwa kwa umbo {*ke*} kutokana mvutano wa irabu ya chini /a/ na irabu ya juu /i/ na kuchukuwa irabu ya kati /e/ kwa vitenzi; *kembi* 'kaimba', *kegizi* 'kaigiza na *kemi* 'kasimama'. Pia nafsi ya tatu umoja ($Nfs_{3u}$) hudokezwa kwa umbo la {*ke*} kutokana na tangamano na irabu; yaani irabu /a/ imebadilika kuwa /e/ kwa vitenzi vyenye mofu {me} yenye kudokeza hali timilifu. Mifano mingine ilivyodhihirika ipo katika Data Na. 8 hapa chini.

(i) *ka- me- lyavy-*a tangamano la irabu /a/→/e/ hali timilifu kemelyavya 'ametowa' $Nfs_{3u}$ $H_{lt}$ $M_{zz}$ $T_{mt}$
(ii) ka-me-lyaw-i- ya tangamano la irabu /a/→/e/ hali timilifu kemelyawiya 'ametokea' $Nfs_{3u}$ $H_{lt}$ $M_{zz}$ $K_LT_{mt}$

**Chanzo:** Data za Uwandani (2022)

Kadhalika, $Nfs_{3u}$ huwakilishwa na mofu {*mwa-*}. Mofu hii hujumuisha mofu tatu kwa pamoja, yaani nafsi ya tatu umoja {$Nfs_{3u}$} wakati uliopita {Njpt} na urejeshi {Rej}. Hali hii ya mofu za nafsi kudokeza mofu tatu kwa pamoja si ya kawaida kujitokeza katika lugha nyingi za Kibantu. Tuchunguze Data Na. 9 kwa ufafanuzi zaidi.

(i) *mwa- pig- w- a* 'aliyepigwa' $Nfs_{3u(nj,rej)}M_{zz}$ Kt $T_{mt}$
(ii) *mwa-vik-a* 'aliyepika' $Nfs_{3u(nj,rej)}M_{zz}$ $T_{mt}$
(iii) *mwa-kw-ambi-a* 'aliyekwambia' $Nfs_{3u(nj,rej)}K_j$ $M_{zz}$ $T_{mt}$
(iv) *mwa-kwend-a* 'aliyekwenda' $Nfs_{3u(nj,rej)}M_{zz}$ $T_{mt}$

**Chanzo:** Data za uwandani (2022)

Data Na. 9 inaonesha mofu {*mwa-*} imefumbata mofu tatu kwa pamoja, yaani inatoa tafsiri ya jumla ya neno 'aliye' (nafsi ya tatu umoja, wakati uliopita na urejeshi wa mtenda). Katika mifano ya (i) na (ii) mofu {mwa} imefuatiwa na shina la kitenzi, - *pigwa* na *–vika* katika mifano ya (iii) na (iv) mofu {*mwa-*} imefuatana na mofu {*ku-*} iliyoyeyusha sauti ya irabu /u/ baada ya kukutana na irabu /a/ na /e/ ikapatikana kiyeyusho /w/ na kufuatiwa na shina la kitenzi -*ambia* na *–enda.*

Pia, Wamakunduchi hutumia mofu {*m-*} kuwakilisha nafsi ya tatu umoja katika vitenzi tofauti. Data za utafiti huu zinaonesha kuwa, mofu {*m-*} inatoa tafsiri ya jumla ya neno 'anaye' na 'atakaye' (nafsi ya tatu umoja, wakati ujao/ uliopo na urejeshi wa mtenda) kutegemeana na njeo iliyofuata baada ya mofu {m}, yaani kama ni wakati uliopo {*na-*} au ujao {*cha-*}. Maumbo haya yote huwapo katika umilisi wa wazawa na hujitokeza katika utendaji katika maana rejelewa. Data Na. 10 inadhihirisha jambo hilo.

(i) *m- na- kut- a* 'anayepata' $Nfs_{3u}$ $N_{jpo\ (rej)}$ $M_{zz}$ $T_{mt}$
(ii) *m- na- vik- a* 'anayepika' $Nfs_{3u}$ $N_{jpo(rej)}$ $M_{zz}$ $T_{mt}$
(iii) *m-cha-ku-o-a* 'atayekuoa' $Nfs_{3u}N_{jjo(rej}$ $K_j$ $M_{zz}$ $T_{mt}$

**Chanzo:** Data za Uwandani (2022)

Data Na. 10 inaonesha dhihirisho la mofu {m-} inayowakilisha nafsi ya tatu umoja (Nfs3u) katika vitenzi vya lahaja ya Kimakunduchi. Mofu hii hujitokeza mwanzoni mwa kitenzi, ambapo pamoja na kuashiria nafsi ya tatu, hubeba pia dhima ya urejeshi wa mtenda katika tungo. Katika mifano ya (i) *m-na-kut-a* 'anayepata' na (ii) *m-na-vik-a* 'anayepika', mofu {m-} inaambatana na mofu ya njeo ya wakati uliopo {na-}, jambo linaloashiria kuwa kitendo kinaendelea kutendeka wakati wa sasa. Kwa upande mwingine, mfano wa (iii) *m-cha-ku-o-a* 'atayekuoa' unaonesha matumizi ya mofu ya njeo ijayo {cha-}, inayoambatana na viambajengo vya kiwakilishi cha yambwa {ku-} na mnyambuliko wa urejeshi {o-}.

Mifano hii inadhihirisha utendaji wa mofu {m-} si tu kama kiwakilishi cha nafsi ya tatu, bali pia kama kipashio muhimu katika kudumisha muundo wa kisintaksia na kimaana wa kitenzi. Jambo hili linaonesha upekee wa lahaja ya Kimakunduchi katika kuwasilisha dhana tata za urejeshi na wakati kupitia mfuatano wa mofu mbalimbali zenye uhusiano wa kifonolojia na kisarufi.

Kadhalika, nafsi ya tatu wingi ($Nfs_{3w}$) katika Kimakunduchi huwakilishwa na mofu {*wa-*} kama ilivyo katika lugha nyingi za Kibantu kikiwemo Kiswahili Sanifu. Umbo {*wa-*} hujitokeza mwanzoni mwa kitenzi katika sura tofautitofauti kama vile {*wa-*} na {*w-*}. Tuchunguze Data Na.11.

(i) *wa- end- a* udomdoshaji wa irabu /a/ →/e/$_{kuwa}$→ *w- end- e* 'wamekwenda $Nfs_{3w}$ $M_{zz}$ Nj
(ii) *wa-os- a* udomdoshaji wa irabu /a/ →/o/$_{kuwa}$→ *w-os-o* 'wamekosha' $Nfs_{3w}$ $M_{zz}$ Nj
(iii) *wa –ang-u* udomdoshaji wa irabu /a/ →/a/$_{kuwa}$→ *w-agu-* 'wameanguka' $Nfs_{3w}$ $M_{zz}$ Nj
(iv) *wa-em-i* udomdoshaji wa irabu /a/ →/e/$_{kuwa}$→ *w- em-i* 'wamesimama' $Nfs_{3w}$ $M_{zz}$ Nj
(v) *wa-cha-vik-a* 'watapika' $Nfs_{3w}$ Wktj $M_{zz}$ $T_{mt}$

**Chanzo:** Data za Uwandani (2022)

Data Na. 11 inaonesha kuwa mofu ya nafsi ya tatu wingi ($Nsf_{3w}$) katika lahaja ya Kimakunduchi huwakilishwa na umbo la msingi {wa-}. Mofu hii hujitokeza katika maumbo tofauti kama {wa}, {w-} au kwa silabi zenye irabu mbalimbali kama {we}, {wo}, {wu}, kulingana na mazingira ya fonolojia na mzizi wa kitenzi husika. Mabadiliko haya hutokana na michakato ya kifonolojia kama vile udondoshaji wa irabu na mvutano wa irabu unaosababishwa na mwingiliano wa sauti zenye sifa zinazokaribiana.

Katika mifano ya (i) hadi (iii), mofu {wa-} hudhihirika kama {w-} kwa sababu ya udondoshaji wa irabu ya awali /a/ pindi inapokutana na irabu nyingine katika mzizi wa kitenzi. Kwa mfano, katika *w-end-e* 'wamekwenda' na *w-os-o* 'wamekosha', udondoshaji hutokea ili kuepuka mfululizo wa irabu zinazofanana, jambo linalorahisisha matamshi. Katika mfano wa (iv) *w-em-i* 'wamesimama', hutokea mvutano wa irabu kati ya irabu /a/ ya mofu {wa-} na irabu /i/ ya mzizi, na matokeo yake ni kutokea kwa irabu ya kati /e/ kutokana na upatanisho wa kifonetiki.

Hali hii inaashiria kwamba katika lahaja ya Kimakunduchi kama ilivyo katika lugha nyingine za Kibantu, mfuatano wa irabu zinazofanana huleta msukumo wa kifonolojia wa kugeuza au kupunguza sauti fulani kwa lengo la kurahisisha matamshi. Katika mfano wa mwisho (v) *wa-cha-vik-a* 'watapika', ambapo mofu ya (Nfs3w) hujitokeza kwa umbo la asili {wa-}, tunashuhudia ulinganifu na Kiswahili Sanifu na lugha nyingine za Kibantu. Hii ni ithibati dhidi ya sarufi ya lahaja ya Kimakunduchi kuwa inadumisha kanuni za kupatanisha sauti na urahisi wa matamshi katika matumizi ya lugha wakati wa mazungumzo ya wazawa.

## 5.0 HITIMISHO

Maelezo tuliyoyaona hapo juu mbali na kubainisha maumbo ya mofu za nafsi katika vitenzi vya lahaja ya Kimakunduchi pia kulikuwa na uchanganuzi wa mabadiliko ya maumbo hayo. Mabadiliko yaliyosababishwa na mazingira husika yaliyokabili baadhi ya sauti za mofu za nafsi kulingana na umilisi na utendaji wa wazawa wa lahaja ya Kimakunduchi. Michakato ya kifonolojia ilioneshwa ili kuyaweka wazi mabadiliko hayo ambayo hayakuathiri usarufi wala usemantiki wa lahaja ya Kimakunduchi. Sambamba na hili makala ilionesha tabia ya uwekevu unaofanywa na Wamakunduchi wakati wa utumiaji wa lahaja yao. Hali iliyowafanya wamilisi wa lahaja tajwa kuficha mofu za nafsi ya kwanza ikiwa katika wakati wa sasa{*na-*} na wakati ujao {*cha-* 'ta-'} kama ilivyooneshwa katika jedwali Na.2 huko juu. Vile vile lahaja ya Kimakunduchi imeonesha uwekevu kwa kujumuisha mofu hususan nafsi ya tatu umoja na mofu nyingine kama vile za njeo na urejeshi katika mazingira maalumu ya kiutendaji kama ilivyooneshwa katika Data Na, 9 na 10 huko juu. Hivyo makala hii imeongeza maarifa kuhusiana na ubainishaji wa maumbo ya mofu za nafsi katika muundo wa kitenzi cha lahaja ya Kimakunduchi kimofosintaksia. Aidha makala hii inatoa mapendekezo kuwa tafiti nyingine zifanyike katika lahaja za Kiswahili na lugha nyingine za Kibantu ili kubaini maumbo ya mofu za nafsi katika miundo ya vitenzi.

## MAREJELEO


- Baker, M. (2008). *The syntax of agreement and concord.* Cambridge University Press.
- Barno, H. (2013) "*Muundo wa Kimofo-sintakisia wa Kitenzi cha Kinandi kwa Mtazamo wa Kiunzi cha Kanuni Finyu*". *Nordic Journal of African Studies. Juz.* 22(4): 213-235. Inapatikana katika *https://www.njas.helsnki. fi/pdf.files*>. Ilisomwa tarehe 30 Juni 2021.
- Bresnan, J., & Mchombo, S. (1987). Topic, pronoun, and agreement in Chichewa. *Linguistic Inquiry, 18*(2), 193–238.
- Charwi, M. (2019) "*Viambishi Nafsi katika Muundo wa Kitenzi Cha Kikuria* (E43*)". Utafiti Juz.*14(2): 339-352. Inapatikana katika *https://www.researchgate.net> publication>339878652*. Ilisomwa tarehe 30 Juni 2021
- Chomsky, N. (1995). *The Minimalist Program.* MIT Press.
- Chomsky, N. (2000). *Minimalist inquiries: The framework.* In R. Martin, D. Michaels & J. Uriagereka (Eds.), *Step by Step: Essays on minimalist syntax in honor of Howard Lasnik* (pp. 89–155). MIT Press.
- Chomsky, N. (2001). *Derivation by phase.* In M. Kenstowicz (Ed.), *Ken Hale: A life in language* (pp. 1–52). MIT Press.
- Embick, D., & Noyer, R. (2001). Movement operations after syntax. *Linguistic Inquiry, 32*(4), 555–595.
- Hamad, S. (2018) Ulinganishi wa Njeo na Hali katika Lahaja za Kipemba, Kitumbatu na Kimakunduchi. Tasnifu ya Uzamivu (Haijachapwa). Zanzibar: Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar.
- Iddi, Z. (2018) Ulinganifu wa Kiisimu katika Kitumbatu na Kimakunduchi. Tasnifu ya Uzamivu (Haijachapwa), Zanzibar: Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar.
- Juma, M. (2019) Ulinganishi wa Mofolojia ya Uambishaji wa Vitenzi kati ya Kimakunduchi, Kitumbatu na Kiswahili Sanifu. Tasnifu ya Uzamivu (Haijachapishwa). Zanzibar: Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar.
- Kihore, Y., Massamba, D. P. Na Hokororo, J. (2012) *Sarufi Miumbo ya Kiswahili Sekondari na Vyuo*. Dar-es-Salaam: Taasisi ya Taaluma za Kiswahili
- Mgullu, R.(1999) Mtalaa wa Isimu. Fonetiki, Fonolojia naMofolojia ta Kiswahili. Kenya: longhorn Publishers Ltd.
- Mohammed, M. A. (2001). *Modern Swahili grammar.* East African Educational Publishers.
- Ngezi, M. (2016) Mfumo wa Njeo na Nafsi katika Vitenzi vya Lugha ya Kihehe. Tasnifu ya Umahiri (Haijachapishwa). Dar es Salaam: Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.
- Radford, A. (1997) *Syntactic Theory and the Structure of English: A minimalist Approach.* New York: Cambridge University Press.
- Schadeberg, T. C. (1992). *A sketch of Swahili morphology.* In B. Comrie & G. G. Corbett (Eds.), *The Slavonic and East European Review, 70*(3), 401–422.
- Vitale, A. (1981). *Swahili syntax.* Foris Publications.
- Wesana-Chomi, E. (2017) *Kitangulizi cha Muundo Viambajengo wa Sentensi za Kiswahili.* Dar es Salaam: TUKI.


**Cite This Article:** Amina Ali Khamis, Devet Goodness Sinyangwe, Dkt. Micheal Amiri Mashauri (2026). Mofu za Nafsi katika Muundo wa Kitenzi cha Lahaja ya Kimakunduchi. *East African Scholars J Edu Humanit Lit, 9*(4), 183-191.